## JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA

### WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI

**MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA**

# TANGAZO

Ofisi ya Usajili (NIDA) Wilaya ya Kyela inatarajia kuongeza wigo wa usajili kwa kuanza kusajili wilaya nzima kwa mfumo wa awamu (Phases) ambapo kila awamu (phase) imepangiwa kanda (zone).

Hivyo, inakaribisha maombi ya ajira ya muda kwa wale wenye sifa stahiki kama ifuatavyo:

**(i) Kazi: Kuingiza Taarifa kwenye Mashine ya Usajili (MEU Operators) (30)**

**Majukumu ya MEU Operator**

1. Kuingiza taarifa za waombaji kwenye mashine za MEU, kuchukua alama za vidole vya waombaji na kuwapiga picha.
2. Kutoa taarifa (kwa Msimamizi) kuhusu takwimu ya idadi ya watu aliowafanyia kazi kila siku baada ya zoezi

**(ii) Sifa za Mwombaji**

1. **Awe na elimu ya kidato cha nne au zaidi.**
2. **Awe na ujuzi wa kutumia Kompyuta**
3. **Umri miaka 18-45**

**(iii) Malipo ni Tsh 10,000/= kwa siku (lazima Operator afikishe fomu 60 kwa siku).**

**Mkataba unaanzia miezi mitatu**

**Maombi yote yatumwe kwa anuani:**

**Ofisi ya Usajili (NIDA)-Kyela**

**c/o**

**Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya,**

**S.L.P 320,**

**KYELA**

**ANGALIZO: Hakuna maombi yatakayopokelewa kwa mkono ama ofisini.**

**MUHIMU: Weka namba yako ya simu**

**Mwisho wa kutuma maombi: 31-08-2017**

**Limetolewa na:**

**K. KAMWELA**

**Afisa Msajili (NIDA),**

**Wilaya ya Kyela**

**k.n.y**

**MKURUGENZI MKUU (NIDA)**